

Ofisi ya Liwali wa Kaunti ya Multnomah

501 SE HAWTHORNE BLVD., Suite 350 • Portland, OR 97214



Huduma yenye mfano bora kwa jamii salama, mwafaka kwa kuishi

**MICHAEL REESE
LIWALI**

**503 988-4300 SIMU
503 988-4500 TTY
www.mcso.us**

Kushughulikia maswala ya usawa katika utekelezaji wa Amri ya Serikali kutoka kwa Gavana Brown

Katika Ofisi ya Liwali wa Kaunti ya Multnomah, tunaamini kuwa kila mtu anapawisa kuhudumiwa kwa njia ya utu na heshima. Maadili yetu kama shirika la utekelezaji wa sheria yanalingana na maadili ya jamii tunayotumikia. Uaminifu wa umma na uwajibikaji katika utekelezaji wa sheria ni muhimu kwa jamii salama na jumuishi. Kama wataalamu wa usalama wa umma na wawakilishi wa jamii tunazotumikia, ni muhimu tuelewe athari inayotokana na shughuli za polisi zinazobagua kwa misingi ya rangi kwa jamii za watu wasio weupe na watu waiotengwa. Hatukubali ubaguzi.

Tunataka kusema wazi, utekelezaji wa [Amri ya Gavana Kate Brown ya "Kaa Nyumbani"](#) unazingatia sheria hii. Maofisa wetu wa liwali wamepokea maelekezo na mwongozo wa kuhakikisha kila mtu anashughulikiwa kwa usawa na heshima. Ili kutoa ufafanuzi wa ziada, Ofisi ya Liwali wa Kaunti ya Multnomah inatoa mwongozo kwa [maswali yanayoulizwa sana](#). Ikiwa mtu anahisi kuwa amedhulumiwa au haki zake zimekiukwa, anaweza kutoa malalamiko akidai utovu wa nidhamu kutoka kwa mshiriki wa MCSO. Malalamiko yanaweza kutoka kwa mtu asiyetaka kujitambulisha au mtu au shirika lingine. Tafadhali fuata hatua zilizo hapo chini.

- MCSO inaweka Fomu ya Malalamiko kwenye tovuti ya shirika (www.mcso.us) iliyo chini ya kichupo cha 'Kutoa Maoni' kwenye ukurasa wa wavuti unaoitwa FAQ. Kulingana na Fomu ya Malalamiko ya MCSO, malalamiko yanapaswa kujumuisha maelezo ya mawasiliano, muhtasari wa tukio linalodaiwa na namna ya jinsi malalamiko yanapaswa kutatuliwa.
- Fomu ya Malalamiko inaweza kuwasilishwa kwa njia zifuatazo, zinazojumuisha lakini sio tu:
 - Wewe mwenyewe kwa mshirika yeyote au katika kituo chochote cha MCSO. Mshirika atasambaza maelezo, kupitia njia zinazofaa, kwa Kitengo cha Mambo ya Ndani.
 - Kwa kupitia faksi kwa Kitengo cha Mambo ya Ndani (503-988-4324).
 - Kwa barua pepe kupitia iau@mcso.us.
 - Kwa kupiga simu kwa Kitengo cha Mambo ya Ndani (503-988-4557).
 - Kwa kutuma barua kwa Ofisi ya Liwali wa Kaunti ya Multnomah.

Malalamiko yote yanayopokelewa yatachunguzwa na Kitengo cha Mambo ya Ndani, na anayelalamika atajulishwa kuhusu matokeo ya uchunguzi. Ofisi ya Liwali wa Kaunti ya Multnomah inachukua malalamiko yote kwa uzito sana, kwani tunajitahidi kuhakikisha uwazi wa polisi, usalama wa jamii na uaminifu wa umma.